# Uenezi wa Kiswahili baada ya Uhuru wa Afrika Mashariki kwa Mtazamo wa Nadharia ya Mifumo Changamano

Susan Chebet-Choge
Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

**Ikisiri**

Kiswahili ni lugha pekee ya Kiafrika ambayo imejinyakulia nafasi ya juu miongoni mwa lugha za kimataifa. Imefikia umataifa huu kutokana na kuenea kwake kijiografia na kimatumizi ndani na nje ya Afrika Mashariki, eneo ambalo ni kitovu chake cha pili hasa cha Kiswahili Sanifu ambayo ni lahaja inayokuzwa kimataifa. Kitovu chake cha kwanza hasa kwa lahaja zake asilia kikiwa mwambao mwa Afrika. Uenezi huu umekuwa wa kasi baada ya nchi za Afrika Mashariki - Tanzania, Uganda na Kenya - kupata uhuru mwanzoni mwa miaka ya 1960. Uhuru huu ulifanya Kiswahili kuenea katika eneo hili hadi kujitwalia hadhi ya kuwa lingua franka. Nchi hizi huru ziliinua hadhi ya Kiswahili kwa njia tofauti; Tanzania iliifanya lugha rasmi, Kenya lugha ya taifa, na Uganda lugha rasmi kwa amri ya Rais mnamo mwaka 1973 (Pawlikova-Vilhanova, 1996). Japo amri hii ya Rais haijatekekezwa hadi sasa, Kiswahili bado kinatumika nchini Uganda kama lugha ya jeshi na polisi na kama lingua franka katika mitagusano ya kibiashara na kijamii. Hadhi hii imesaidia kuenezea Kiswahili ndani na nje ya Afrika. Japo uenezi huu una motisha, haibainiki wazi jinsi shughuli za ujenzi wa mataifa haya zilivyokuza uenezi wake hadi kuufikisha kiwango cha kimataifa katika miongo mitano pekee ikizingatiwa kuwa, si nchi zote zilizoweka mikakati ya kuikuza. Kwa kuwa uenezi wake umefungamana na shughuli za kimaendeleo katika mataifa haya, makala hii imechunguza uenezi wake kwa mtazamo wa Nadharia ya Mifumo Changamano.

## 1.0 Utangulizi: Kiswahili na Hadhi yake

Kiswahili ni lugha ya Kibantu ya jamii ya Niger-Congo na ambayo imeainishwa na *Ethnologue* kama ISO 639-3: SWA (Lewis, 2009). Asili yake ni mwambao mwa Afrika Mashariki (Chiraghdin na Mnyampala, 1977; Choge, 2008). Ni lugha iliyo na majukumu mengi ndani na nje ya Afrika. Ni lugha ya kitaifa, kimatumizi na kikatiba katika nchi za Kenya, Tanzania na Burundi. Vilevile, ni lugha rasmi kikatiba katika nchi za Tanzania, Kenya, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (katika makala hii kuanzia hapa imerejelewa kama JAKIKONGO). Nchini Kenya, Kiswahili ni lugha rasmi kufuatia amri ya Rais iliyotolewa mwaka 1973

(ijapokuwa amri hii haijatekelezwa wala kubatilishwa). Ni lingua franka katika nchi hizi zote na katika sehemu za jirani zao kusini mwa Afrika hususan Msumbiji, Malawi na Zambia (Moshi, 2006; Chebet-Choge, 2012). Hata kabla ya kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki (katika makala hii kuanzia hapa imerejelewa kama JAFRIMA), Kiswahili kilifikishwa nchini Sudan Kusini na wakimbizi wa kisiasa waliorudi nchini mwao baada ya kuishi nchini Kenya kwa zaidi ya miongo miwili. Wakimbizi hao walijifunza Kiswahili katika mitagusano yao na Wakenya na watoto wao wakajifunza pia shuleni na vyuoni (Choge, 2008). Pia, Kiswahili kinasemwa kwa viwango tofauti katika sehemu za kusini mwa nchi ya Uhabeshi, mwambao mwa Afrika Mashariki kuanzia eneo la Mogadishu nchini Somalia hadi mdomo wa mto Lurio nchini Msumbiji na katika visiwa katika mwambao huu kama vile Madagaska, Zanzibar, Pemba, Lamu, Komoro na Ushelisheli japo kwa viwango tofauti (Pawliková-Vilhanová, 1996; Choge, 2009). Makala hii inalenga kuchunguza kwa mtazamo wa mifumo changamano uenezi huu wa Kiswahili kuanzia kitovuni mwake katika mwambao mwa pwani ya Afrika Mashariki ambamo Kiswahili kilitumika kama lugha asilia na jamii ya Waswahili hadi kufikia hadhi yake ya kisasa ya kimataifa. Makala hii imegawanyika katika sehemu nne ambazo ni utangulizi, nadharia iliyoongoza uchambuzi wa makala, harakati zilizokuza uenezi wa Kiswahili baada ya uhuru wa nchi za Afrika Mashariki na mwisho ni hitimisho.

**2.0 Nadharia**

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Mifumo Changamano (Elman, 1995; Finch, 2004; Larsen-Freeman, 2008; van Geert, 2008; Marin na Peltzer-Krapf, 2009; Hayes na Andrews, 2020). Nadharia hii huchunguza mifumo changamano, isiyonyoofu, yenye ugiligili mwingi, ambayo sehemu zao huingiliana na kuathiriana. Hali ya kuingiliana na kuathiriana huendelea kati ya sehemu zote za mfumo hadi mfumo mzima uathirike. Mifano ya mifumo hii ni kitu, mtu, taasisi, mwenendo, tabia, nchi na lugha.

Makala hii imechunguza mambo yaliyoeneza Kiswahili tangu nchi za Afrika Mashariki zilipopata uhuru hadi kufika kiwango cha kimataifa. Makala imejengwa kwa msingi wa nadhariatete kuwa uenezi wa lugha ni mfumo changamano ulio hai na wenye kubadilikabadilika. Ukuaji na uenezi wa lugha huathiriwa na shughuli za kueneza mifumo mingine ambayo mwishowe husababisha kuenea kwa Kiswahili. Hata kabla ya uhuru, Kiswahili kimekuwa sehemu ya maisha ya Waafrika katika Afrika Mashariki kwa karne nyingi kikichukua nafasi muhimu katika biashara, masuala ya dini na usafiri. Baada ya uhuru, nchi za Afrika Mashariki, hasa Kenya na Tanzania, zilikuza Kiswahili kwa kuifanya lugha ya taifa katika harakati za kujenga na kukuza utaifa kutoka kwa watu wa makabila tofauti. Makala hii inachukulia

kuwa uenezi wa Kiswahili kijiografia na kimatumizi ndani na nje ya Afrika Mashariki baada ya uhuru ulitokea kwa kiwango kikubwa kutokana na mikakati iliyowekwa na nchi hizo kukuza mifumo mingine ya maendeleo. Kwa kuwa mifumo yote ya nchi imeingiliana, mikakati hii ilikuza na kueneza Kiswahili pia. Katika mtazamo wa mifumo changamano, kitu chochote kinachoathiri mfumo mmoja huathiri mifumo mingine, mwishowe, kuathiriana huku husababisha mfumo mzima kuathirika (Chebet-Choge, 2010; Kirumba, 2015).

## 3.0 Harakati Zilizoeneza Kiswahili baada ya Uhuru wa Nchi za Afrika Mashariki

Uhuru wa nchi za Afrika Mashariki ni mojawapo ya misukumo iliyokuza na kueneza Kiswahili ndani na nje ya Afrika kwa njia tofauti. Misukumo mingine ni mikakati ya kuunda na kukuza utaifa kutoka makoloni yaliyojinyakulia uhuru, elimu, biashara, ufufuzi na upanuzi wa JAFRIMA. Misukumo hii imejadiliwa katika sehemu zifuatazo.

### 3.1 Mikakati ya Kuunda na Kukuza Utaifa

Uhuru wa nchi za Tanzania, Uganda na Kenya uliopatikana mnamo 1961, 1962, na 1963 mtawalia, uliweka majukwaa mbalimbali yaliyokuza na kueneza Kiswahili kijiografia na kimatumizi ndani na nje ya Afrika. Baada ya uhuru, harakati za kuunda utaifa kutoka kwa makabila tofauti ya nchi hizi zilianza (Mulokozi, 2002; Legère, 2006). Marais Nyerere na Kenyatta waliona Kiswahili kama gundi ya kushikanishia makabila tofauti katika nchi zao ili kuunda mataifa. Iliaminiwa kuwa lugha nyingi huleta utengano baina ya watu, kwa hivyo, mataifa mengi ya Afrika yalilenga kukuza lugha moja ambayo ingetumiwa na watu wote (Bamgbose, 1994). Mnamo mwaka 1969, bunge la Kenya lilipitisha hoja ya Kiswahili kufanywa lugha ya taifa ifikapo mwaka 1970. Aidha, mwaka 1970 chama tawala cha KANU kikapitisha kuwa ifikapo mwaka 1974 Kiswahili kiwe lugha rasmi ya Kenya. Hata hivyo, Kiswahili hakikupewa taji hili la utaifa na urasmi hadi mwaka 1974 Rais Kenyatta alipotumia mamlaka yake ya urais kuitangaza lugha ya taifa (Mazrui na Mazrui, 1995). Baada ya matangazo hayo, Kiswahili kilianza kutumika bungeni. Hivi majuzi ukuzaji na uenezi huu wa Kiswahili kupitia matumizi yake bungeni ulipata kipaumbele wakati bunge lilipozindua tarehe machapisho ya kanuni za kudumu za bunge katika Kiswahili tarehe 12 Novemba, 2020 ili kiweze kutumiwa bungeni sambamba na Kiingereza (Parliament of Kenya, 2020). Japo chama cha KANU kilipendekeza Kiswahili kiwe lugha rasmi ifikapo 1974, Kiswahili hakikupata hadhi ya urasmi hadi mwaka 2010 kilipoidhinishwa kikatiba kuwa mojawapo ya lugha rasmi za Kenya.

Rais Nyerere naye aliendeleza Kiswahili na kukifanya sehemu muhimu ya Watanzania. Aliendeleza falsafa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kutumia istilahi za Kiswahili. Aliwaita Watanzania *ndugu*, na viongozi wengine kote duniani waliokuwa na mtazamo wa kisoshalisti kama yeye. Alitumia neno *ujamaa* kama njia ya kusisitiza umoja wa Watanzania. Yeye alijiita *mwalimu*, jina lililoakisi kazi yake ya awali ya ualimu na kazi yake wakati huo ya kuelekeza Watanzania kama rais (Chebet-Choge, 2012). Alipanua msamiati wa Kiswahili kwa kuibua istilahi *ng'atuka* kwa kuitohoa kutoka lugha ya Kizanaki. Kwa hivyo, Kiswahili kilianza kuwa sehemu ya utamaduni wa Watanzania (Blommaert, 1994; Legère, 2006).

Nchini Kenya, Kenyatta pia alitumia istilahi ya Kiswahili *harambee* kuwatia shime Wakenya ili wafanye bidii katika ujenzi wa taifa kwa kushirikiana. Aliwapa maadui wa Kenya majina ya Kiswahili: *ujinga*, *umaskini* na *ugonjwa*. Maadui hawa wangeshindwa iwapo Wakenya wangeshirikiana pamoja kupitia mwito wa *harambee*. Rais Moi naye alifuata nyayo za Rais Kenyatta za kutumia Kiswahili katika uongozi wake. Falsafa ya mtindo wake wa kisiasa ilipewa jina la Kiswahili *nyayo* na pia mwito wake wa kuweka taifa pamoja ulikuwa, *umoja*, *amani* na *upendo*. Kiswahili pia kimetumika katika kuyapa majina majengo na taasisi za serikali kama vile *Jogoo House* (jumba la Wizara ya Elimu), *Fedha House* (jumba la Wizara ya Fedha), *Sheria House* (jumba la Wizara ya Sheria), *Kilimo House* (jumba la Wizara ya Kilimo), *Harambee House* (jumba lenye Ofisi ya Rais) na *Nyati House* (jumba lenye ofisi mbalimbali za serikali).

### 3.2 Nafasi ya Elimu

Licha ya suala la utaifa, utekelezaji wa sera za elimu umeeneza Kiswahili kijiografia na kimatumizi. Tangu uhuru kupatikana, Kiswahili kimekuwa sehemu ya masomo ndani na nje ya Afrika Mahariki katika viwango vyote vya elimu japo ufundishaji wake haujawa sawa katika nchi zote. Nchini Tanzania, Kiswahili ni somo katika ngazi zote za elimu na lugha ya kufundishia masomo yote katika shule za chekechea na za msingi isipokuwa masomo ya Kiingereza na lugha zingine. Ndivyo ilivyo nchini Kenya, Kiswahili hufunzwa na kutahiniwa pia hutumiwa kufundishia kozi za Kiswahili katika vyuo vikuu. Japo Kiswahili kinafunzwa katika shule za msingi na za upili nchini Uganda, si somo la lazima kusomwa na kutahiniwa katika shule zote na kwa wanafunzi wote, isipokuwa katika vyuo vya walimu vya stashahada na katika vyuo vikuu kwa wale wanaosomea Kiswahili[1] (Lodhi, 1993; Amidu, 1995; Blommaert, 1994; Mukama, 2004; Swilla, 2009).

Nchini Kenya, katika mfumo wa elimu wa 8-4-4, Kiswahili ni somo la lazima kusomwa na kutahiniwa katika shule za msingi na sekondari. Pia, kimepewa

[1] Katika miaka ya 1970 Kiswahili kilikuwa kikitahiniwa katika shule za upili.

hadhi kubwa ya kuwa mojawapo ya masomo matatu ya msingi - Hisabati, Kiingereza na Kiswahili - ambayo sharti yajumuishwe wakati wa kuamua gredi ya mwanafunzi katika mitihani ya kitaifa ya shule za msingi na sekondari. Kiswahili hufunzwa kuanzia kiwango cha chekechea hadi vyuo vikuu na ni lugha ya kufundishia masomo yote katika shule za chekechea zenye wanafunzi mchanganyiko kiisimu. Kiswahili hutumiwa kufundishia somo la Kiswahili katika ngazi zote za elimu. Kufuatia mapendekezo ya Tume ya Mackey ya mwaka 1981, Chuo Kikuu cha Moi mjini Eldoret kilianzishwa kama chuo kikuu cha pili nchini Kenya kikipendekeza Kiswahili kama mojawapo ya lugha zitakazofunzwa katika idara iliyopendekezwa kuwa ya Kiswahili na Lugha Zingine za Kiafrika. Jukumu kubwa la idara hii ni kutayarisha walimu wa Kiswahili watakaofunza katika shule za upili, vyuo vya astashahada na stashahada na katika vyuo vikuu. Chuo hiki ni cha kwanza nchini Kenya kufundisha Kiswahili kwa kutumia Kiswahili, tofauti na ilivyokuwa katika Chuo Kikuu cha Nairobi[2] kilichokuwa kikifundisha kwa kutumia Kiingereza.

Tangu kuanzishwa kwa chuo hiki hadi sasa, Idara ya Kiswahili na Lugha Zingine za Kiafrika inazidi kukuza Kiswahili kwa mapana kupitia utayarishaji wa walimu wa Kiswahili ambao wengi wao wamechukua nafasi kubwa katika kuendeleza Kiswahili ndani na nje ya Afrika Mashariki. Baadhi ya walimu wa Kiswahili waliokuwa wa kwanza kufuzu kutoka chuo hiki ni: Prof. Inyani Simala, Katibu Mtendaji wa Kwanza wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki; Prof. Nathan Ogechi ambaye kwa sasa ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Moi na mtaalamu wa Kiswahili wa kutambulika kimataifa; Dkt. Susan Chebet Choge ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro; Dkt. Mahiri Mwita ambaye ni Mhadhiri wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Princeton, Marekani na mmoja wa wadau wakuu katika kuendeleza Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU). Kwa sasa, asilimia 100% ya Wakenya waliopitia mfumo wa elimu wa 8-4-4 wana umilisi na utendaji wa viwango vya juu katika Kiswahili. Kadiri idadi hii inavyoongezeka ndivyo idadi ya wale walio na umilisi finyu inavyozidi kupungua. Elimu itazidi kukuza Kiswahili ndani na nje ya Kenya kwa kuwa nafasi hii muhimu iliyotolewa katika mfumo wa 8-4-4 imeimarishwa katika mfumo mpya wa elimu wa 2-6-6-3 ulioanzishwa mwaka 2017. Mfumo huu unasisitiza umilisi na utendaji wa masomo yote.

[2] Chuo Kikuu cha Nairobi kilikuwa chuo kikuu pekee nchini Kenya wakati huo, Chuo cha Moi kilikuwa cha pili.

### 3.3 Nafasi ya Biashara

Shughuli za kiuchumi zimechukua nafasi muhimu katika kueneza Kiswahili kijiografia na kimatumizi kwa karne nyingi. Kama ilivyo kabla ya uhuru, Kiswahili bado ni lingua franka katika biashara za kisasa kama vile za kunadi bidhaa sokoni, fedha, uchukuzi na usafirishaji katika JAFRIMA. Nchini Kenya, mojawapo ya sekta ambayo imekuza Kiswahili katika harakati za kukuza biasahara zake ni benki. *Vitemahela*[3] vya benki zote vina maelezo katika Kiingereza na Kiswahili ya namna ya kuweka na kutoa pesa. Mfano wa maelezo haya katika Kiswahili ni: *Tafadhali ingiza kadi yako*. Benki hizi zimezipa bidhaa zake majina ya Kiswahili, kwa mfano, benki ya Absa[4] ina akaunti za *Pepea* na *Uwezo* nayo Kenya Commercial Bank (KCB) ina akaunti za *Mapato*, *Masomo*, *Simba* na *Mavuno*. Benki hii pia imekuwa na mashindano ya kifedha tangu mwaka 2009 yaliyopewa majina ya Kiswahili kama vile *Nguruma tena na KCB*, *Shinda acre na KCB* na *Weka weka na upate acre na KCB* (Chebet-Choge, 2012).

Ukuzaji wa biashara za sekta ya utoaji wa huduma za simu katika Afrika Mashariki pia umeeneza Kiswahili kijiografia na kukikuza kimatumizi kwa kuzitangazia na kuzipatia majina bidhaa na taasisi zake za kifedha. Baadhi ya makampuni hayo ni Safaricom (Kenya), Tigo (Tanzania), Vodacom na MTN (Uganda, Rwanda, Burundi na Tanzania), na Airtel (Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi). Nchini Kenya, kampuni ya Safaricom imekuza Kiswahili kwa kuzipatia bidhaa na huduma zake majina ya Kiswahili ikianzia kwa jina lake lenye neno la Kiswahili *safari*. Kaulimbiu yake *Nawe kila wakati* imo katika Kiswahili pia. Vilevile, bidhaa nyingi za kampuni hii zina majina ya Kiswahili kama vile *MPESA* (njia ya kutuma na kupokea pesa kwa simu), *MKesho* (akaunti ambayo mtu hutoa na kuweka pesa kupitia simu). Mofu {m-} katika majina haya inasimamia neno 'mobile' ambalo limetumiwa kuwakilisha rununu. Hivyo basi, jina *MPESA* lina maana ya 'pesa kwenye rununu.' Majina mengine ya Kiswahili ya bidhaa za kampuni hii ni *okoa jahazi* (mkopo wa fedha za kununua muda wa maongezi), *skiza tunes* (soko la kuuza sauti za simu) na *bonga points* (mradi wa kuwazawadia watu kulingana na viwango vya pesa zilizowagharimu katika kutumia huduma zake), *sambaza* (huduma inayotumiwa kugawanyia mtu hela za kupigia simu) na *M-Shwari* (huduma ya benki kwenye rununu). Vilevile, kampuni hii ina *info kiosk* (duka katika rununu la kuuza habari tofautitofauti), *Lipa na M-PESA* (huduma inayotumiwa kufanyia malipo kupitia simu) (Chebet-Choge, 2012; Sandy, 2015; Safaricom, 2020).

---

[3] *Vitemahela* ni istilahi ambayo nimeibuni kurejelea mashine zinazotumiwa kutoa pesa benkini kwa kutumia kadi (ATM), umoja ni *kitemahela*.

[4] Awali iliitwa *Barclays*.

Kwa sasa Kampuni hii ya Safaricom ina bidhaa mpya za *okoa data* (huduma inayotoa mkopo kwa ajili ya kununua data ya kutumiwa mtandaoni) na *Fuliza* (huduma ya kutoa mkopo kwa minajili ya kutuma kwa *MPESA*). Japo neno hili *fuliza* lina sura ya Kiswahili, kifonolojia halikuwa katika Kiswahili kabla ya kuibuliwa na kampuni hii. Kiswahili kina neno *fulika* lenye maana ya 'ishiwa na pesa ama filisika'. Kampuni hii ilifanya uhandisi wa kiisimu na kuunda neno *fuliza* kama kinyume chake. Katika muktadha wa matumizi yake, *fuliza* lina maana ya 'jazwa ama pokezwa pesa.' Vilevile, neno hili lina uhusiano kisemiotiki na neno *puliza* lenye maana ya 'tia pumzi' ama 'vuvia.' Jinsi mtu anavyopuliza kwa kutumia mdomo ama kifaa kingine kuweka pumzi, kwa mfano, moto ili uwake vyema au mpira na magurudumu ya magari ili yaweze kutumiwa, vivyo ndivyo huduma hii ya *fuliza* inavyompatia mtu uwezo wa kutimiza malengo yake kwa kumkopesha pesa za kutuma. Kampuni hii pia ina *Zuri* (mhudumu wake wa kidijiti mtandaoni anayeshughulikia wateja wanaotafuta habari kuhusu huduma inazozitoa katika rununu) na ina *Lipa Mdogo Mdogo* (huduma ya kuuzia wateja wake rununu kwa mkopo ambao wataulipia kwa shilingi ishirini za Kenya kila siku) katika bohari ya huduma zake ya *544# runununi (Safaricom, 2020)[5].

Nchini Tanzania, makampuni ya kutoa huduma za simu hukuza Kiswahili pia kupitia biashara zake. Licha ya makampuni haya kutumia Kiswahili kama lingua franka ya biashara zake, makampuni haya yamezipa majina ya Kiswahili bidhaa na huduma zake. Kwa mfano, kampuni ya Vodacom ina huduma ya *Soko Letu* (huduma ya kupata habari za spoti za ligi za kandanda na kuchuuza bidhaa za spoti), *Songesha* (huduma ya kuwezesha wateja kutuma pesa kupitia huduma ya M-PESA hata kama hawana pesa za kutosha katika akiba zao), *M-Koba* (huduma kwa vikundi vidogovidogo kama vile VICOBA) na *Pindua Pindua* (aina ya kifurushi cha rununu kinachotumiwa kwa kutekeleza shughuli tofauti kama vile kupiga simu, kusaguza mtandao na kutuma jumbe) na *Halal Pesa* (huduma ya mtandao inayomwezesha mteja kuongeza na kutumia pesa zake kulingana na kanuni za Uislamu za Sharia) (Vodacom, 2020).[6]

Makapuni mengine ya simu nchini Kenya na Tanzania hutumia pia Kiswahili katika kukuza biashara zake na kutoa huduma za simu kama wafanyavyo Safaricom na Vodacom. Maoni ya Coulmas (1992) ni kwamba lugha ni njia pia ya kuzalisha mali basi si ya kumilikiwa tu. Makampuni haya yametoa muhtasari wa uhusiano kati ya Kiswahili na biashara katika Afrika Mashariki. Hivi sasa ni vigumu kuendeleza biashara katika eneo hili pasipokutumia Kiswahili.

---

[5] Katika www.safaricom.co.ke imesomwa tarehe 3 Novemba, 2020.

[6] Katika www.vodacom.co.tz imesomwa tarehe 6 Novemba, 2020.

### 3.4 Nafasi ya JAFRIMA

Kufufuliwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAFRIMA) mnamo mwaka 2000 miaka ishirini na mitatu tangu ilipovunjika mwaka 1977, ni tukio lililoeneza Kiswahili kwa kiasi kikubwa kijiografia na kimatumizi ndani na nje ya jumuiya hii. JAFRIMA hii mpya ina nchi sita kwa sasa ambazo ni: Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda, Burundi na Sudan Kusini (State Department of East Africa Affairs, 2016). Kulingana na ripoti ya World Population Review juu ya makadirio ya idadi ya watu ulimwenguni kwa mwaka 2020, idadi ya wanaJAFRIMA ni takriban milioni mia mbili. Uanachama wake utazidi kupanuka iwapo maombi ya JAKIKONGO na Somalia kujiunga nayo yatakubaliwa (Mugisha, 2019; Kirugu, 2019). Nchi ya Uhabeshi pia imedhihirisha nia ya kujiunga nayo. Iwapo itajiunga nayo, basi nchi za Eritrea na Jibuti huenda zikavutwa kujiunga nayo pia. Kujiunga kwa nchi hizi kutaongeza idadi ya watu katika JAFRIMA kufikia milioni mia tatu. Kwa kuwa ni sharti muhimu kwa kila mwanachama kuimarisha Kiswahili kama lingua franka miongoni mwa raia wake, kujiunga kwa nchi hizi kutafanya JAFRIMA kuwa eneo moja kubwa lenye wasemaji wengi wa Kiswahili duniani na kufanya lugha ya Kiwahili kuongeza idadi ya wasemaji wake kwa kasi. Ukuzaji wa Kiswahili kama lingua franka katika nchi wanachama ni jukumu ambalo JAFRIMA imeitwika KAKAMA[7] (EAC, 2008).

Sharti hili la kufanya lazima nchi mwanachama kukuza Kiswahili kama lingua franka miongoni mwa raia wake, limekuwa nyenzo muhimu katika ukuzaji na uenezi wa Kiswahili. Limefanya Rwanda na Burundi kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi na ya taifa sambamba na Kinyarwanda na Kirundi (Bishumba, 2017). Vilevile, limetoa msukumo kwa nchi ya Sudani Kusini kufundisha Kiswahili katika shule zake (Kiunguyu na Guardian Reporter, 2019). Kila nchi mwanachama inahitajika kuunda Baraza la Kitaifa la Kiswahili ambalo litafanya kazi kwa ushirikiano na Tume ya Kiswahili ya JAFRIMA katika kukuza Kiswahili kwenye nchi wanachama (EAC, 2008). Tanzania tayari ina BAKITA (Baraza la Kiswahili la Taifa) lililoundwa mwaka 1967, Kenya na Uganda zimo katika harakati za kuunda mabaraza yake. Nchini Kenya, mswada wa kuunda baraza lake umo katika hatua ya kuwasilishwa bungeni na nchini Uganda, baraza la mawaziri liliidhinisha mwaka jana kubuniwa kwa baraza hili nchini humo (Cabinate Office, 2019 na *Daily Monitor*, 2019). JAFRIMA ni soko kubwa mno, na yeyote anayenuia kuwekeza hapa, hana budi kujifunza na kukuza Kiswahili kwa kuwa ni ufunguo wake kwa soko hili. Nafasi hii ya Kiswahili katika maendeleo ya Afrika Mashariki ilitabiriwa na Mwalimu Nyerere katika hotuba yake ya mwaka 1960 katika Chuo Kikuu cha

[7] Ni ufupisho wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Hii ni tume ya iliyobuniwa na JAFRIMA ili kukuza ulingua franka wa Kiswahili katika nchi wanachama.

Duquesne, nchini Marekani aliposema, “Kiswahili ni lugha pekee yenye nguvu za kuunganisha nchi zote za Afrika Mashariki” (Legère, 2006:377).

### 3.5 Mwamko wa Uanaafrika[8] Uliolenga Kubuniwa kwa Taifa Moja la Afrika

Mwamko wa Uanaafrika umekuwa jambo mojawapo linalotoa msukumo uliofanya Kiswahili kuenea kijiografia na kimatumizi. Waanzilishi wa mataifa ya Afrika kama vile Kwame Nkrumah wa Ghana, Nnamdi Azikiwe wa Nigeria na Julius Nyerere wa Tanzania walitazamia kuundwa kwa *taifa moja* la watu wenye *nia moja* na *lugha moja*. Walitazamia Kiswahili kiwe lugha ambayo wangeifanya kuwa rasmi ya taifa hili lililotarajiwa kuundwa pindi tu nchi zote za Afrika zitakapopata uhuru (Chebet-Choge, 2012). Matamanio haya yalisababisha Kiswahili kufunzwa katika nchi za Ghana na Libya. Nchini Ghana, Kiswahili kilianza kufunzwa katika Chuo Kikuu cha Ghana kuanzia mwaka 1964 na mojawapo ya wanafunzi waliofuzu masomo ya Kiswahili kutoka chuo hiki ni Prof. Assibi Amidu wa Chuo Kikuu cha Trondheim nchini Norway. Fauka ya kuwa Profesa wa Kiswahili anayetambulika kimataifa, ameandika makala na vitabu kadha vya Kiswahili (Amidu, 1995; Amidu, 2007). Nchini Libya, Hayati Muhamar Gadhafi aliyekuwa rais wa nchi hiyo alikuwa amejitolea kwa hali na mali kufanikisha uundaji wa taifa moja la Afrika na mkakati mmoja aliotumia ni kukuza Kiswahili nchini mwake. Katika utawala wake, Kiswahili kilifunzwa katika vyuo na shule mbalimbali. Kilifunzwa katika vyuo vikuu vya Sebha, Al Fateh na Nasser. Hivi sasa kuna Walibya ambao wamehitimu shahada za uzamivu katika Kiswahili. Kabla ya kuangushwa kwa uongozi wake, Libya ilikuwa ikitangaza kazi za ufundishaji wa Kiswahili (Wesana-Chomi, 2008). Amidu anaeleza kuwa Kiswahili kilifunzwa katika Chuo Kikuu cha Port Harcourt nchini Nigeria kuanzia mwaka 1979 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990 kilipoachwa kutokana na ukosefu wa wahadhiri (Dzahene-Quarshie, 2013). Umoja wa Afrika ulikipa Kiswahili jukwaa muhimu la kuenezwa kijiografia na kimatumizi ndani na nje ya bara la Afrika wakati ilipokiidhinisha kuwa mojawapo ya lugha zake rasmi (African Union, 2003). Hotuba ya kwanza katika Kiswahili kwa umoja huu ilitolewa mwaka 2004 na Rais Chissano wa Msumbiji (Chebet-Choge, 2012).

Hatua ya kufanya Kiswahili kuwa mojwapo ya lugha rasmi za Umoja wa Afrika ilimotisha nchi, taasisi na watu wenye nafasi kubwa katika nchi zao kuidhinisha ufundishaji na matumizi yake. Asasi ya kwanza kufuata mkondo huu ni SADC ambayo mwaka 2016 ilikiidhinisha Kiswahili kuwa mojawapo ya lugha zake rasmi kando na Kireno, Kiingereza na Kifaransa kama njia ya kutambua mchango wa Hayati Mwalimu Nyerere katika ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika

[8] Mwamko wa Uanaafrika umetumiwa kurejelea *Pan-Africanism*.

(SADC, 2019; Nhongo, 2019). Tamko hili lilipitishwa na SADC katika kikao chake cha marais cha 39 kilichofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 17-18 Agosti 2019 (The Guardian Reporter, 2019). Nchi za Sudan Kusini na Afrika Kusini zimeidhinisha Kiswahili kifunzwe katika shule zao kuanzia mwaka 2020 na hivi karibuni, nchi ya Bostwana imefuata mkondo huu (Khumalo, 2018; Language Magazine, 2020; Lang'at, 2020).

Uamuzi wa kufundisha Kiswahili Afrika Kusini ulifuata mwito uliotolewa awali na aliyekuwa kiongozi wa vijana katika chama cha ANC Bw. Julius Malema[9] wa kufanya Kiswahili kama lugha ya kuunganisha Waafrika (Ngcobo, 2018). Licha ya Malema, Kwame Appiah Boateng, mwanaharakati wa mwamko wa Uanaafrika kutoka Ghana, amependekeza chama cha kwanza cha kisiasa cha taifa nuiwa huru la Afrika alichokiita *Uhuru Africa Convention*. Ametumia neno la Kiswahili *uhuru* kwa kuwa yeye, kama mwana mwamko wa Uanaafrika, anaamini kuwa Kiswahili ni kitambulisho cha Waafrika wote duniani. Kwa maoni yake, Kiswahili kitawashikamanisha na kuwaleta Waafrika pamoja. Jina *uhuru* linadhihirisha ukombozi kamilifu wa Waafrika (Chebet-Choge, 2012).

Hivi sasa, kuna *ombi la haki* linaloendelezwa mtandaoni la kushinikiza Umoja wa Mataifa kuidhinisha Kiswahili kama mojawapo ya lugha zake rasmi, ombi hili likitetewa kwa misingi minne ambayo ni: (i) Kiswahili ni lugha ya JAFRIMA, (ii) eneo la Afrika Mashariki lina makambi makubwa duniani ya wakimbizi wanaotumia Kiswahili, (iii) idhinisho la serikali ya Afrika Kusini la kufunzwa Kiswahili nchini humo kuanzia mwaka 2020 ni ishara kuwa Kiswahili kinakumbatiwa na Afrika na (iv) makao makuu ya Programu ya Mazingira (UNEP) ya Umoja wa Mataifa yamo jijini Nairobi nchini Kenya; nchi ambayo ni kitovu cha Kiswahili (IDEA AFRICA, 2019).

Mwamko huu wa kukumbatia Kiswahili barani Afrika umetiwa kasi na maelewano yaliyoafikiwa kati ya KAKAMA na ACALAN[10] katika mkutano uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 26-28 Juni, 2019. Katika mkutano huo, taasisi hizi mbili zilikubali kushirikiana katika kutambua na kustawisha Kiswahili kama lingua franka na lugha ya kukuzia maendeleo ya kudumu barani Afrika (Dar es Salaam Framework for Action, 2019). Hali ilivyo sasa, Kiswahili kinaendelea kuenea kijiografia na kupanuka kimatumizi duniani. Kwa mujibu wa Choge (2008),

---

[9] Bw. Malema ni mwanasiasa mwenye ushawishi mkubwa hasa miongoni mwa vijana Afrika Kusini. Awali, alikuwa kiongozi wa vijana katika chama cha ANC na kwa sasa ni kiongozi wa chama cha Economic Freedom Fighters (EFF) (Ngcobo, 2018).

[10] ACALAN ni ufupisho wa African Academy of Language. Hii ni taasisi ya Jumuiya ya Afrika iliyobuniwa ili kushughulikia ukuzaji na uhifadhi wa lugha za Afrika.

Kiswahili ni lugha ambayo idadi ya watu wanaoitumia inaongezeka kwa kasi mno kushinda lugha yoyote ulimwenguni.

### 3.6 Nafasi ya Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari vimechangia kwa kiwango kikubwa kueneza Kiswahili kwa kuitumia katika vipindi mbalimbali. Vyombo vilivyochukua nafasi kubwa ni redio, runinga na magazeti. Hivi sasa, wavuti na mitandao ya kijamii imeanza kuchukua nafasi muhimu katika uenezi wa Kiswahili. Utangazaji wa redio kwa kutumia Kiswahili umekuza Kiswahili kwa miongo mingi ndani na nje ya Afrika kupitia katika vipindi vyake. Nchini Kenya, kuna Shirika la Utangazaji la Kenya (*Kenya Broadcasting Corporation* (KBC), *Idhaa ya Kiswahili* na *Redio Maisha*. Nchini Rwanda, kuna *Redio Rwanda* ambayo imekuwa ikitangaza kwa Kiswahili tangu mwaka 1961 (Yusufu, 2004). Nchini Uganda, matangazo ya redio katika Kiswahili yalianza mwaka 1971 lakini hayakushika kasi kwa sababu yalipata pingamizi kubwa. Kwa sababu hiyo, redio zilizo na vipindi vya Kiswahili nchini Uganda ni chache na hutoa vipindi vyake kwa muda mfupi mno vikilinganishwa na vya Kenya na Tanzania. Baadhi ya redio hizi nchini Uganda ni *Redio West* inayotoa matangazo ya michezo kwa Kiswahili na *Redio Uganda* inayotoa matangazo ya habari kwa Kiswahili[11].

Licha ya matangazo ya redio katika JAFRIMA, *Redio Cairo* hutangaza kwa Kiswahili tangu mwaka wa 1950 (Brennan, 2008). Katika visiwa vya Komoro, Kiswahili kilianza kutumika katika matangazo ya redio tangu mwaka 1975 (Omar, 2004). Vituo vingine vinavyotangaza kwa Kiswahili nje ya bara la Afrika ni *Redio Moscow Kimataifa*, *Redio Deutsche Welle*, *Sauti ya Marekani* (Voice of America (VOA)), *Shirika la Utangazaji la Uingereza* (British Broadcasting Corporation (BBC)), *Redio Japani Kimataifa*, *Redio Sudani*, *Redio Irani*, *Redio India*, *Redio Kimataifa ya Ufaransa*[12] na *Redio Uchina Kimataifa* (Kiango, 2005; RFI, 2010; Yang, 2011).

Nchini Kenya, runinga pia hukuza Kiswahili katika matangazo yake japo kwa ufinyu ikilinganishwa na redio. Japo kuna vituo vingi vya runinga nchini humo ni vitano pekee vilivyo na vipindi katika Kiswahili sanifu. Vituo hivi ni Shirika la Utangazaji la Kenya (Kenya Broadcasting Corporation (KBC)), *Kituo cha Televisheni cha Nation* (Nation Television (NTV)), *Kituo cha Televisheni cha*

[11] Nilipata habari hii kutoka kwa Bi Dorcas Wanyama tarehe 02 Julai, 2020. Bi Wanyama ni mdarisi wa Kiswahili katika chuo kimoja cha stashahada nchini Uganda na pia ni mwanafunzi mzamili anayesomea shahada ya Elimu ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Masinde Muliro nchini Kenya.

[12] Radio France Internationale.

*Citizen* (Citizen Television (CITIZEN)), *Kituo cha Televisheni cha Mfumo Mtandao wa Kenya* (Kenya Televison Network (KTN)) na *Kituo cha Televisheni cha Kenya 24 (*Kenya 24 Television (K24)). Vituo hivi vyote hutoa matangazo ya habari ya saa moja jioni katika Kiswahili na asubuhi kuanzia saa kumi na moja hadi saa mbili asubuhi. Vipindi hivyo vya habari katika Kiswahili ni *NTV Jioni, Citizen Nipashe,* KBC *Darubini,* KTN *Leo* na K24, Vilevile, vituo hivyo hurusha vipindi vya Kiswahili vya alfajiri vya *NTV Afajiri*, *KBC Pambazuka* na *NTV Jarida la Jimbo* (Chebet-Choge, 2012).

Uchapishaji wa magazeti na majarida katika Kiswahili umekuza na kueneza pia Kiswahili. Tanzania ndiyo nchi inayoongoza duniani katika uchapishaji wa magazeti ya Kiswahili. Takriban asilimia 75% ya magazeti nchini humo yanaandikwa kwa Kiswahili. Baadhi ya magazeti hayo ni *Mwanaspoti, Mtanzania, Mzalendo, Mwananchi* na *Nipashe.* Nchini Kenya uchapishaji wa magazeti ya Kiswahili unazidi kudidimia. Hivi sasa, ni gazeti la *Taifa Leo* pekee ndilo lililosalia kinyume na ilivyokuwa hapo awali ambapo kulikuwapo pia magazeti mengine kama *Kenya Leo, Taifa Jumamosi* na *Taifa Jumapili*. Japo idadi ya magazeti ya Kiswahili imedidimia, matumizi ya Kiswahili katika magazeti yanayochapishwa kwa Kiingereza takriban yote yameongezeka. Baadhi ya magazeti hayo ni *The Daily Nation, Saturday Nation, Sunday Nation, The Standard, Saturday Standard, Sunday Standard, Nairobian, The Star* na *The People.* Baadhi ya maandishi ya Kiswahili katika magazaeti haya ni tangazo la IEBC[13] juu ya upigaji kura Agosti 2017 '*TUMIA KURA YAKO KUKATA KIU YAKO AUG 8$^{TH}$ #WEWENDIOKUSEMA*' (*Sunday Nation*, Julai 30, 2017, uk. 7), '*mama Sospeter akipata job itabidi ukuwe mwanamume kamili* (*Sunday Nation*, Septemba 8, 2019, uk. 10) na '*vaa kiatu kabla ya kuingia ugani kucheza*' (*Nairobian,* Septemba 6-12, 2019, uk. 35) na matumizi ya maneno ya Kiswahili kama vile *tujuane, zoezi* na *fundi* (*Sunday Nation,* Novemba 1, 2020, uk. 9).

Aidha, tovuti na mitandao ya kijamii ni TEHAMA iliyorahisisha mawasiliano, kwani imekuwa ni bohari na masoko makubwa ya kuhifadhi na kunadia bidhaa zozote. Fauka ya majukumu haya TEHAMA hizi ni maktaba kuu za makala na marejeleo ya maandishi ya aina tofauti, ikiwamo Kiswahili. Hivi sasa, vitabu vingi na machapisho mengine ya Kiswahili pamoja na habari tofauti juu yake zimo mtandaoni. Kuna kamusi kadha za kidijiti za ujozi-lugha mtandaoni kati ya Kiswahili na lugha zingine, nyingi zikihusisha Kiingereza. Mifano ya kamusi hizi ni *Swahili-English* Dictionary (TshwaneDJe Software and Consulting, *n.d*), *English-Swahili Dictionary* (Schroeter and Uecker, *n.d*), *TUKI English-Swahili/Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili* (TUKI, 1996), *Swahili-Kiingereza/Kamusi ya Kiswahili-*

[13] IEBC ni akronimi ya Independent Electoral and Boundaries Commission.

*Kiingereza* (TUKI, 2001), *Swahili-Italian* iliyoundwa na Prof. Madalena Tuscano wa Chuo Kikuu cha Naples na *Kamusi Project: Internet Living Kiswahili Dictionary* ya Chuo Kikuu cha Yale (YPAL[14], 1994; Kiango, 2005).

Vilevile, maduka ya kuuza vitabu mtandaoni yamekuza na kueneza Kiswahili ulimwenguni. Duka la Amazon.com lina mamia ya vitabu vya Kiswahili. Baadhi ya vitabu hivyo ni *Saa ya Ukombozi* (Nkwazi Nkuzi Mhango), *Barua Ndefu Kama Hii* (Mariama Ba), *Kamusi Sanifu ya Kiswahili* (cha TUKI), *Kamusi ya Kiswahili-English* (John C. Rigdon), *Modern Swahili Grammar* (M.A. Mohammed) na *Mtalaa wa Isimu* (Richard Mgullu). Licha ya vitabu vinavyochuuzwa mtandaoni kuna pia mamia ya tasnifu na maelfu ya makala za Kiswahili katika majarida kazi hizi nyingi husomwa bila malipo yoyote.

Halikadhalika, programu nyingi za kutekeleza shughuli mbalimbali za lugha mtandaoni zinachangia ukuzaji na uenezi wa Kiswahili ulimwenguni. Baadhi ya programu hizi ni: *English to Kiswahili Translator 3.0* ambayo ni ya kufanyia tafsiri kutoka na kwenda Kiswahili, *TuKsi Koti la Rangi* ambayo ni programu ya kuchorea kwa watoto na nyingine ni *jambo spellchecker* ambayo ni ya kusahihishia tahajia (Chebet-Choge, 2012 ).

Aidha, kampuni za *Google*, *Microsoft* na *Twitter* zinakuza na kueneza Kiswahili kimataifa kwa kuasilisha[15] programu katika Kiswahili na lugha zingine za kiasili duniani. Kupitia uasilishaji huu, kampuni ya *Twitter* imeweza kuunda programu ya kutafsiri habari kutoka kwa lugha zingine hadi Kiswahili. Ufanisi huu ulifikiwa kufuatia *ombi la haki* lililoendeshwa mtandaoni na watumiaji wa *Twitter* chini ya *#SwahiliISNotIndonesian* (Oludimu, 2018). Vilevile, *Google* ina mtindo wa Kiswahili wa *kusaguza*[16] mtandao na programu ya kutafsiri kwa Kiswahili na kutoka Kiswahili kwa lugha zingine (Chin, 2009). *Microsoft* nayo imetafsiri programu zake za *Microsoft Office* kwa Kiswahili kwa kuwa Kiswahili ni lugha yenye nafasi kubwa katika Afrika Mashariki (Phombeah, 2004).

Uandishi wa vitabu vya fasihi kama njia moja ya kujadili masuala ibuka ndani na nje ya Afrika umechangia kwa kiasi kikubwa kueneza Kiswahili. Baada ya uhuru, fasihi nyingi zilizoandikwa katika Kiswahili zilisawiri masuala ibuka kama vile ukoloni mamboleo, udikteta wa viongozi katika Afrika huru, matatizo ya wafanyakazi, ukabila, masuala ya jinsia, utandawazi, magonjwa ibuka kama vile UKIMWI, korona, uongozi mbaya serikalini uliojaa ufisadi na upendeleo, na

[14] YPAL inasimamia Yale Programme in Africa Languages.
[15] *Asilisha* ni istilahi ambayo nimetumia kueleza ule mchakato wa kuandika programu ya kompyuta kwa lugha asilia mbalimbali, kwa Kiingereza mchakato huu huitwa *localize*.
[16] *Saguza* ni istilahi ambayo nimeitumia kurejelea dhana ya *search the web* katika Kiingereza.

kuanguka kwa taasisi muhimu. Jedwali lifuatalo linaonesha baadhi ya vitabu vya fasihi ya Kiswahili vilivyomo mtandaoni na masuala ibuka vinavyoyashugulikia.

**Jedwali Na. 1: Masuala Ibuka katika Vitabu vya Kiswahili Vilivyomo Mtandaoni**

| Na. | Masuala Ibuka Yanayoshughulikiwa | Kitabu na Mwaka wa Uchapishaji | Mwandishi |
|---|---|---|---|
| 1. | Masuala ya ukoloni-mamboleo, uongozi mbaya katika Afrika, ukabila. | *Kinjeketile* (1969), *Mashetani* (1971), *Ngao ya Jadi* na *Jogoo Kijijini* (1976) zote ni tamthilia | Ibrahim Hussein |
| | | *Chozi la Heri* (2018) riwaya | Asumpta K. Matei |
| 2. | Masuala ya wafanyakazi | *Sauti ya Dhiki* (1973) ushairi | Abdillatif Abdallah |
| | | *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (1979) riwaya | Shafi Adam Shafi |
| | | *Kilio cha Haki* (1981) tamthilia | Al Amin Mazrui |
| | | *Visiki* (1981) tamthilia | Khaemba Ongeti |
| | | *Sikate Tamaa* (1982) ushairi | Said A. Mohamed |
| 3. | Masuala ya ukabila, ufisadi na ubadhirifu serikalini, utegemezi wa misaada ya kutoka nje na miundo misingi duni ya matibabu na kilimo, uongozi mbaya | *Amezidi* (1997) tamthilia | Said A. Mohamed |
| | | *Walenisi* (1995) riwaya | Katama Mkangi |
| | | *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi zingine* (2016) hadithi fupi | Said A. Mohamed |
| 4. | Masuala ya utandawazi | *Bina-Adamu* (2001) riwaya | Kyalo Wamitila |
| | | *Dunia Yao* (2006 riwaya | Said A.Mohamed |
| 5. | Masuala ya kijamii kama vile UKIMWI, jinsia na matabaka katika jamii, matumizi ya madawa ya kulevya miongoni mwa wanafunzi, uchafuzi wa mazingira | *Unaitwa Nani?* (2008) riwaya | Kyalo Wamitila |
| | | *Kigogo* (2016) tamthilia | Pauline Kea |

**Chanzo:** Mwandishi wa makala (2020)

**4.0 Hitimisho**

Makala hii imedhihirisha kuwa uenezi wa Kiswahili kijiografia na kimatumizi kimataifa baada ya uhuru wa nchi za Afrika Mashariki umefungamana na maendeleo katika sekta mbalimbali za nchi hizi kama vile uundaji na ukuzaji wa utaifa, elimu, bisahara, kufufuliwa na kupanuliwa kwa JAFRIMA, mwamko wa Uanaafrika na upanuzi wa matumizi ya Kiswahili katika TEHAMA mbalimbali. Katika harakati za kuimarisha sekta hizi, Kiswahili kimeimarishwa pia. Sababu hizi zimekuwa na nguvu zaidi katika ukuzaji wa Kiswahili kwani zimewafanya watu ndani na nje ya Afrika Mashariki kujifunza na kutumia Kiswahili. Wanachama wa JAFRIMA pia wamesukumwa na masharti mawili ya mkataba ulioibuni jumuiya hii. Sharti la kwanza limo katika kifungu 119(d) ambalo linahimiza ukuzaji wa Kiswahili kama sehemu ya utamaduni wa nchi mwanachama na la pili limo katika kifungu 137(2) linalohitaji Kiswahili kukuzwa kama lingua franka katika nchi zote za jumuiya. Masharti haya mawili yamekuwa sababu kubwa ya kuenea kwa Kiswahili ndani ya JAFRIMA kwa kuwa nchi wanachama takriban zote zimeidhinisha Kiswahili kuwa lugha rasmi au lugha ya taifa. Masharti haya yamelazimisha kuundwa kwa mabaraza ya Kitaifa ya Kiswahili katika kila nchi mwanachama ili yashirikiane na KAKAMA katika kukuza Kiswahili kimatumizi kama lingua franka katika JAFRIMA. Kama nilivyoeleza awali, KAKAMA imeingia katika makubaliano na ACALAN kueneza Kiswahili barani Afrika kama njia ya kutekeleza azimio la Umoja wa Afrika la kukifanya Kiswahili kuwa mojawapo ya lugha zake rasmi. Uenezi wa Kiswahili ndani na nje ya JAFRIMA utaendelea kwa sababu kukijua na kukitumia Kiswahili ni kuzalisha mali, kukuza utaifa, kuweka usalama, kuweka mitagusano, kuimarisha umoja kati ya mataifa, kurahisisha mawasiliano, usafirishaji na uchukuzi kati ya watumiaji wake.

**Marejeleo**

African Union. (2003). "Protocal on the Amendments to the Constitutive Act of the African Union." Katika https://au.int/en/treaties/protocal-amendments-constitutive-act-africa-union. Imesomwa Septemba 14, 2019.

Amazon.com (n.d). Swahili Books. katika www.amazon.com/books-swahili.

Amidu, A. A. (1995). "Kiswahili, a Continental Language: How Possible Is It? (Part I)." *Nordic Journal of African Studies*. 4(2): 50-70.

Amidu, A. A. (2007). "Kiswahili, a Continental Langaue: How Possible Is It? (Part 1)." *Nordic Journal of African Studies*. 4(2): 50-70.

Amidu, A. A. (2007). *Semantic Assignment Rules in Bantu Classes*. Cologne: Rudiger Köppe Verlag.

Bamgbose, A. (1994). "Pride and Prejudice in Multilingualism and Development." Katika R. Fardon & G. Furniss (Eds.), *African Languages, Development and the State* (pp 33-43). London: Routledge.

Batibo, H. M. (2000). "The Linguistic Situation of Tanzania." Katika K. Kahigi, Y. Kihore, & M. Mous (Eds.). *Lugha za Watanzania* (pp. 5-17). Leiden: CNWS, Leiden University.

Bishumba N. (2017). "MPs Approve Law Making Swahili Official Language." *The New Times*. katika www.newtimes.co.rw/section/read/207840. Imesomwa Septemba 13, 2019.

Blommaert, J. (1994). "The Metaphor of Development and Modernization in Tanzanian Language Policy and Research." Katika R. Fardon & G. Furniss (Eds.), *African Languages, Development and the State* (pp. 213-225). London: Routledge.

The Language Magazine.com. (2020). "Botswana to Introduce Swahili Language in Local Schools." *The Language Magazine*, katika http://www.languagemagazine.com/2020/10/12/botswana-to-introduce-swahili-language-in-local-schools/. Imesomwa Novemba 02, 2020.

Brennan, J. R. (2008). Poison and Dope: Radio and the Art of Political Invective in East Africa, 1940-1965. Paper presented at the African Studies Center Seminar, University of Leiden, 15 May.

Cabinate Office (2018). "Establishment of the National Kiswahili Council. Third Cabinate Meeting held on 4th August, 2018." Nairobi, Kenya, katika https://www.president.go.ke/2018/08/14/third-cabinet-meeting-held-on-14th-august-2018. Imesomwa Septemba 10, 2019.

Chebet-Choge, S. (2010). "Towards Understanding Language Death. The Case of Dead and non-used Nandi Anthroponyms." *Alternative*. 6(1): 38-53.

Chebet-Choge, S. (2012). "Fifty Years of Kiswahili in Regional and International Development." *The Journal of Pan African Studies*. 4 (10): 172-203.

Chin, J. (Septemba, 3, 2009). "Google now available for Swahili and African." *Google in Sub-Saharan Africa: news, stories and thoughts*. katika https://africa.googleblog.com/2009/09/google-translate-now-available-for.html. Imesomwa Septemba 14, 2019.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Choge, S. (2009). "Understanding Kiswahili Vowels." *The Journal of Pan African Studies*. 2(8): 62-77. katika http://www.jpanafrican.com/. Imesomwa Machi 15, 2018.

Choge, S. C. (2008). "Role of [a] in Kiswahili". *Research in African Languages & Linguistics*. 8: 19-43.

Coulmas, F. (1992). *Language and Economy*. Oxford: Blackwell.

Daily Monitor (2019). "Uganda Govt Endorses Council to Promote Adoption of Kiswahili." *The East African.* katika www.theeasafrican.co,ke/. Imesomwa Septemba 14, 2019.

Dzahene-Quarshie, J. (2013). "Ghana's Contribution to the Promotion of Kiswahili: Challenges and Prospects for the African Unity." *Journal of Pan African Sudies*. 6(6): 69-89.

East Africa Community (2016). *The History of the EAC*. katika www.eac.int/eac-history. Imesomwa Novemba 07, 2020.

East Africa Community. (1999). *The Treaty for the Establishment of the East African Community (Amended 2007)*. Arusha: East African Community. katika www.eala.org. Imesomwa Septemba 14, 2019.

East Africa Community. (2008). Protocol on the Establishment of the East Africa Kiswahili Commission. Arusha.

Elman, J.L. (1995). "Language as a Dynamical System." katika Robert F. Port & T van Gelder (Eds.) *Mind as motion: Explorations in the dynamics of cognition*. Cambridge, MA: MIT Press. (pp. 195-223). Katika http://crl.ucsd.edu/~elman/Papers/dynamics/dynamics.html. Imesomwa Machi 10, 2010.

Fabian, J. (1986). *Language and Colonial Power: The Appropriation of Swahili in the Former Belgian Congo 1880-1938*. Berkeley: University of California Press.

Finch, A. (2004). "Complexity and Systems Theory: Implications for the EFL." *Journal of Asia TEFL*. 1(2):27-46.

Hayes, A.M. and Andrews, L.A. (2020). "A Complex Systems Approach to the Study of Change in Psychotherapy." *BMC Medicine.* KIJITALI[17] katika https://doi.org/10.1186/s12916-020-01662-2. Imesomwa Septemba 14, 2019.

IDEA AFRICA (2019). "Fanya Kiswahili Moja ya Lugha Rasmi za UN (Make Sawhili one of the UN official languages)". katika www.change.org/p/united-nations-fanya-kiswahili-kuwa-moja-ya-lugha-rasmi-ya-un-make-swahili-one-of-the-un-official-languages. Imesomwa Julai 15, 2020.

Khumalo, Thuso. (2018). "South African Schools to Teach Kiswahili in 2020." *VOANEWS.* katika www.voanews.com/africa/south-africa-schools-teach-kiswahili-2020. Imesomwa Julai 15, 2020.

Kiango, J.G. (2005). "Tanzania's Historical Contribution to the Recognition and Promotion of Kiswahili. Special Survey Article 1/2005." *Africa and Asia No 5*. Dept. of Oriental and African Languages: Göteborg University, pp 157-166. katika www.sprak.gu.se Imesomwa Mei 12, 2018.

Kirugu, M. (2019). "East Africa is the Fastest Region for the Fifth Straight Year, DRC & Somalia ask to join EAC." *The Africareport*. katika www.theafricareport.com/14066/east-Africa. Imesomwa Septemba 13, 2020.

Kirumba, M. R. (2015). Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Isimujamii katika Shule za Sekondari Nchini Kenya. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia.

Kiunguyu, K. & Guardan Reporter. (2019, May 30). "Tanzania to Send Kiswahili Teachers to South Sudan." *IPPMEDIA*. katika https://ippmedia.com/en/features/tanzania-send-kiswahili-teachers-south-sudan. Imesomwa Septemba 13, 2019.

Lang'at, P. (2020, January 11). "Kiswahili Goes to School in South Africa." *The East African*. katika www.theeastafrican.co.ke/tea/news/east-african/kiswahili-goes-to-school-in-south-africa-1434586?view=htmlamp. Imesomwa Oktoba 27, 2020.

Larsen-Freeman, D. and Cameron, L. (2008). *Complex Systems and Applied Linguistics*. Cambridge: Oxford University Press.

Legère, K. (2006). "JK Nyerere of Tanzania and the Empowerment of Kiswahili." Katika M. Putz, J. A Fishman, Neff-van Aertselaer (Eds.) '*Along the*

[17] KIJITALI ni akronimu ya Kitambulisho Cha KidiJITALI ambayo nimeitumia kwa maana ya DOI/doi

*Routes to Power'. Explorations of Empowerment through Language*. Berlin: Mouton de Gruyter. pp 373-403.

Lewis, P.M. (Ed.). (2009). *Ethnologue: Languages of the World* (16th Ed). Texas: SIL International. katika http://www.ethnologue.com/. Imesomwa Mei 21, 2018.

Lodhi, A. Y. (1993). "The Language Situation in Africa Today." *Nordic Journal of African Studies*. 2(1): 79–86.

Marin, M.M. and Peltzer-Karpf, A. (2009). "Towards a Dynamic Systems Approach to the Development of Language and Music: Theoretical Foundations and Methodological Issues." Katika Louhivuori, J. et al (Eds.), *The 7th Triennial Conference of European Society for the Cognitive Sciences of Music (ESCOM)*. pp. 284-292. Katika https://jyx.jyu.fi/. Imesomwa Machi 15, 2018.

Mburu, S. (2019). "Tafakari: Vaa Kiatu kabla ya Kuingia Ugani Kucheza." *Nairobian*. Nairobi: Standard Media Group. Uk. 35.

Moshi, L. (2006). "The Globalised World Languages: The Case of Kiswahili." Katika F. A. Olaoba and M. A. Pemberton (Eds.). *Selected Proceedings of the 36th Annual Conference on African Linguistic* (pp. 166-175). Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project. Katika www.lingref.com, Document #1421.. Imesomwa Julai 05, 2011.

Mugisha, I.R. (2019). "DR Congo Entry into EAC will be a game Changer." *The East African.* katika www.theeastafrican.co.ke/news/ea/DR-Congo-entry-into-EAC. Imesomwa Septemba 13, 2020.

Mukama, Ruth. (2004). "Uendelezaji, Ukuzaji na Usambasaji wa Kiswahili Uganda." Katika S.A.K Mlacha (Mh.). *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki* (pp. 12-25). Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M.M. (2002). "Kiswahili as a National and International Language." katika www.abibitumikasa.com/yabb/Attachments/kiswahili.pdf. Imesomwa Julai 05, 2011.

Muriuki, K. (Novemba 1, 2020). "Honouring my Kenyan Roots with my Passion for Fitness. Life Style." *Sunday Nation*. Nairobi: Nation Media Group. p. 10.

Mwalimu Andrew (2019, Septemba 8, 2019). "Staffroom Diary: Why I'II allow Fiona to be with Fisi Alex. Life Style." *Sunday Nation*. Nairobi: Nation Media Group. p. 10.

Ngcobo, K. (2018). "Malema Wants Language to Unite Africans as Kiswahili gets dept's nod." *Independent Online*. katika www.iol.co.za/news/south-

africa/malema-wants-language-to-unite-africans-as-kiswahili-gets-depts-nod-17141694. Imesomwa Septemba 14, 2019.

Nhongo, K. (2019). "SADC Council Recommends Adoption of Kiswahili. Southern Research and Documentation Centre." katika www.sardc.net/net/en/southern-african-news-features/sadc-council-recommends-adoption-of kiswahili/. Imesomwa Septemba 14, 2019.

Oludimu T. (2018). "Swahili Becomes the First African Language to be Recognized by Twitter." katika http://technopoint.africa/2018/05/08/twitter-recognise-swahili. Imesomwa Septemba 14, 2019.

Omar, A. B. (2004). "Utumiaji wa Kiswahili Nchini Komoro." Katika S.A.K Mlacha (Mh.). *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki*. Dar es Salaam: TUKI. Kur. 12-25.

Parliament of Kenya. (2020). "Bunge la Taifa Kutumia Kiswahili katika Mijadala Bungeni." katika http://www.parliament .go.ke/bunge-la-taifa-kutumia-kiswahili-katika-mijadala-bungeni. Imesomwa 15 Novemba, 2020.

Pawliková-Vilhanová, V. (1996). "Swahili and the Dilemma of Ugandan Language Policy." *Asian and African Studies*. 5(2): 158–170.

Phombeah, G. (2004). "Microsoft to Launch in Kiswahili. BBC Africa." katika http://news.bbc.co.uk/2/hi/africa/3816717. Imesomwa Septemba 14, 2019.

RFI. (2010). "RFI Launches Kiwahili Service in Ten Countries." *Radio France Internationale*. katika www.rfi.fr. Imesomwa Novemba 07, 2020.

SADC. (2019). Communique of the 39th ADC Summit of Heads of State and Governement (No. 17). Held at Julius Nyerere International Convention Centre, Dar es Salaam, United Republic of Tanzania. August 17-18. katika www.sadc.int/. Imesomwa Septemba 14, 2019.

Sanday, W. A., (2015). "Evaluating the Acceptance and Usability of Kiswahili Localized Mobile Phone App In Kenya: A Case of M-Pesa App." *The Journal of Specialised Translation*.

Schroeter, A. and Uecker, P. (n.d). *English-Swahili*. Katika https://en.bab.la/dictionary/english-swahili. Imesomwa Novemba 11, 2019.

State Department of East Africa Affairs (2016). Editorial: "South Sudan's Admission into the EAC-Opportunities and Challenges." *Jumuiya News*. 32: 6-9.

Swilla, I. N. (2009). "Languages of Instruction in Tanzania: Contradictions between Ideology, Policy and Implementation." *African Study Monographs*. 30(1): 1-14.

TATAKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

The Guardian Reporter. (2019). "SADC Adopts Kiswahili as Fourth Official Language." *The Guardian.* katika www.ippmedia.com/en/news/sadc-adopts-kiswahili-fourth-official-language. Imesomwa Novemba 11, 2020.

TUKI. (2000). TUKI English-Swahili dictionary/Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili. Toleo la Pili Dar es Salaam: TUKI. katika www.elimuyetu.co.tz/subject/arts/eng-swa/index.html

TUKI. (2001) Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza/Swahili-English dictionary. Toleo la Kwanza. Dar es Salaam: TUKI. katika www.elimuyetu.co.tz/subject/arts/swa-eng/index.html.

van Geert, P. (2008). The Dynamic Systems Approach in the Study of L1 and L2 Acquisition: An Introduction. *The Modern Language Journal*. 92(2): 179-199.

Wesana-Chomi, E. (2008). *Upatanisho wa Vivumishi na Majina ya Kiswahili*. Sebha: Chuo Kikuu cha Sebha.

World Population Review. (2020). "2020 World Population by Country." Katika https://worldpopulationreview.com/countries. Imesomwa Novemba 11, 2020

Yang, Z. (2011). "CRI's Kiswahili Broadcast Celebrates 50 Years on Air." *The Chinese and African Dream.* katika www.chinafrica.cn/exclusives/txt/2011-09/08/content_389281.htm. Imesomwa Novemba 05, 2020.

YPAL, (1994). "Kamusi Project: Internet Living Swahili Dictionary." Yale University: Yale Programme in African Languages. katika https://books.google.com/books/about/The_Kamusi_Project.html?id=BBJ7WEACAAJ. Imesomwa Septemba 14, 2019.

Yusufu, M.A. (2004). "Matumizi ya Kiswahili redio Rwanda, Kigali." Katika S.A.K Mlacha (Mh). *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki*. Dar es Salaam: TUKI. kur. 12-25.